
Moja ya basi la mwendokasi la UDART.

# UDART inabemendwa?

Na Allan Lawa

PENYE miti hapana wajenzi. Kauli hii ni moja ya misemo ya Kiswahili kuonesha ukengeufu katika kutumia raslimali watu na mali, ndani ya taasisi katika kutanzua mambo yanayoizonga jamii.

Usemi huu unasadifu kwa yanayotokea kwenye mradi wa mabasi yaendayo haraka jijini Dar es Salaam – BRT au DART, Uswahilini maarufu kama mabasi ya mwendokasi.

Mradi wa BRT ulianza kazi Mei 10, 2016, miaka karibu 10 sasa, ukiwa na lengo kuu moja; kuwapa wakazi wa Dar es Salaam usafiri wa uhakika wakati wote wa kwenda kwenye shughuli zao za ujenzi wa Taifa na kurejea majumbani.

UDART, ulikuwa mradi wa mfano kwa nchi 54 za Bara la Afrika. Baadhi ya nchi zilikuja kuona na kujifunza jinsi ya kujenga miundombinu na baadaye uendeshaji wake. Shirika la Fedha Duniani (IMF), liliusifu mno mradi huu.

Baada ya kukamilika ujenzi wa miundombinu, mabasi, tena kwa idadi kubwa yaliingizwa kutoka nje. Pia kulikuwa na ahadi ya kuongeza mengine mara kwa mara.

Hata hivyo, utoaji huduma katika mradi huu umeshuka kwa kiwango kikubwa, kutokana na mabasi kupungua, lakini na usimamizi dhaifu ndani ya vituo, hasa kituo kikuu cha Kimara Mwisho.

Baada ya miaka karibu 10 sasa, tulitarajia matatizo ya mwanzo wa kila kitu kipya, yangelikuwa yamekwisha au yamesalia kidogo. Hata hivyo hali haiko hivyo DART, kwani Kimara Mwisho, hasa nyakati za asubuhi, ni vurugu tupu. Hali iko vivyo hivyo nyakati za jioni wakati watu wanarejea makwao.

Utaratibu wa kuingia kwa mistari umekwisha na sasa wenye nguvu tu ndio wanaoingia mwanzo bila kujali watoto, wanawake na wazee, tena si kwa kupitia milangoni bali kwenye madirisha. Hii inatokana na idadi kubwa ya abiria hasa asubuhi, ambapo kila mmoja anataka kuwahi kazini au kwenye biashara zake.

Hali hii inaonesha kuwa wenye dhamana ya uendeshaji wa DART hawajui tabia ya wateja au watu wanaowahudumia. Nina hakika kama wangelikuwa wanajua tabia ya wanaowahudumia, wangeongeza idadi ya mabasi nyakati hizo.

Sina hakika kama menejimenti inasema 'wacha wafilie mbali'. Kauli iliyowahi kutolewa miaka ya nyuma na kiongozi mmoja mkuu kulipotokea shida ya usafiri nchini.

Tabia ya kupitia madirishani ilikuwapo miaka ya nyuma Mbagala, ambako usafiri wa daladala ulikuwa mgumu mno. Ninaambiwa kutokana na ugumu wa usafiri wakati huo, wanawake wa huko walilazimika kuvaa kaptula ili kukabiliana na ubabe wa kuingia kupitia madirishani.

Waingereza wana usemo wao, kuwa ukitaka kumwua mbwa mpe jina baya. Kwa kuwa DART naipenda, sitaki kuipa jina baya. Ninatamani kuipa menejimenti jina, lakini ninasita kwa kuwa ninaamini watabadilika na kurejea kwenye lengo la mradi.

Lengo la mradi huu lilikuwa kuwapa usafiri wa uhakika wakazi wa Dar es Salaam na maeneo ya pembezoni mwa Jiji kama Kibaha, ili kuchapuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Wakati mradi unakabiliwa na mazonge haya, miundombinu yake inapita ndani ya eneo la kilometa moja, ya moja ya vyuo maarufu vya usafirishaji Kusini mwa Jangwa la Sahara, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

DART inashindwa vipi kutumia hazina iliyopo ndani ya NIT? Kama haiwezi kuajiri wahitimu na kwa hakika haiwezi kuajiri wote kutoka taasisi hii, bado inaweza kuitumia kama mshauri mwelekezi, ili kuondokana na mkwamo uliopo kwenye mradi.

NIT iliyoanzishwa miaka 50 iliyopita, ina sifa ya pekee ya ubora wa ufundishaji katika sekta ya usafiri na uchukuzi Kusini mwa Jangwa la Sahara. Inafundisha wataalamu wa usafirishaji wa ndani na nje. Inatoa kozi hadi Shahada katika sekta ya usafiri na usafirishaji

Tuna wahitimu wengi wa chuo hiki, lakini sina hakika kama ndani ya DART wapo, na kama wapo sina hakika kama wanatumika au kama wanasikilizwa kikamilifu. Inawezekana kuwa pamoja na kuhitimu, labda viwango vyao ni vya chini mno.

Kama kuna shida ya weledi miongoni mwa wahitimu basi, DART iongee na NIT ili kurekebisha mtalaa wake, ili kukidhi mabadiliko ya mahitaji ya sekta ya usafiri na usafirishaji nchini.

Nina hakika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila katika kituo kikuu cha DART Kimara Mwisho, ilisukumwa na picha mjongeo kwenye mitandao zikionesha abiria wakiingia ndani ya mabasi kupitia madirishani, kutokana na kilichoelezwa kuwa ni uhaba wa mabasi asubuhi.

Haitoshi kwa Chalamila kusema aliyosema kwa kuilaumu menejimenti ya DART kushindwa kuongeza mabasi na kuilinganisha hatua hiyo na hujuma kwa Serikali na wananchi wanaotumia mabasi hayo.

Chalamila alikwenda mbali zaidi, kuwa Serikali haitasita kuchukua hatua kali, kama ulegevu wa utoaji huduma ndani ya DART utaendelea. Hii ni kauli ya kisiasa zaidi, kwani uhaba wa mabasi na msongamano wa abiria kwenye vituo, ni vya muda mrefu.

Mkuu wa Mkoa pia ameitisha menejimenti ya DART kuwa ataichongea kama itashindwa kutanzua vurugu kwenye vituo, ili hatua kali zilichukuliwe dhidi yake pamoja na kuondolewa kazini, ili kulinda maslahi ya wananchi wake.

DART kuna tatizo, kwani mara kadhaa mabasi yanajaza abiria kupita kiasi na wakati mwingine gari linatembea tupu, tena kwa mwendo mrefu kwa maelezo mepesi, kuwa dereva amemaliza muda wake, anakwenda kumwachia dereva mwingine wa zamu.

Hivi ni kweli Watanzania hatuna uwezo wa kuendesha biashara hata kwenye mazingira ya ukiritimba, kama ilivyo kwa usafiri wa DART? Njia yanakopita mabasi haya daladala zimepunguzwa, na pia yana njia ya pekee ili kuyaepusha na misongamano ya njiani.

DART hii inayoonekana imechoka, kama atapewa mtu binafsi na mwekezaji huyu akaamua kurithi wafanyakazi au hata menejimenti, utashangaa kwa jinsi ilivyokuwa kutakavyokuwa na mabadiliko makubwa na ufanisi wa utendaji kazi.

Watanzania tuamke, tuthamini chetu kwa kukilinda kwa wivu mkubwa na kwa kufanya kazi kwa bidi. Hivi kweli tunataka kuruhusu hata kazi chache zilizoko DART, nazo zipotee kama ilivyokuwa kwenye zaidi ya viwanda 400 vilivyobinafisishwa na vingine kuuzwa na vingi kufungwa baada ya hapo. Hapana. Nimeamua kusema tu.

CamScanner

KERO



**BAADHI ya waendesha boda boda wamekua na tabia ya kubeba mizigo ya nondo na kuziburuta katika barabara jambo linaloleta uharibifu.**

CamScanner

Uhuru Jumatano Agosti 20, 2025 Pg 16




**MWENDESHA pikipiki akiwa amebeba abiria na mizigo bila kujali usalama wake na abiria, Kinondoni Dar es Salaam, jana. (Picha na Jumanne Gude).**

CamScanner